

MKATABA WA KUPANGISHA YARD (ENEO LA KUPAKI MAGARI)

Mkataba huu umefanyika leo tarehe...mwezi wa JANUARY mwaka 2024.

BAINAYA

NDUGU MATONYANGE TRANSPORT LTD wa S.L.P 304 MOSHI (ambaye katika mkataba huu atajulikana kama "MPANGISHAJI" neno ambalo litamhusu yeye mwenyewe, warithi wake, mawakala wake, na yeyote ambaye atakuwa anadai haki katika mkataba huu, mwenye nyumba.) kwa upande mmoja.

NA

Ndugu, THOMAS SAVUTU MSOFE T/A SAVUTU HARDWARE wa S.L.P 7284 ARUSHA (Ambaye katika mkataba "MPANGAJI" neno ambalo litamhusu yeye binafsi, mrithi wake, mawakala wake na yeyote ambaye atakuwa anadai haki katika mkataba huu) kwa upande wa pili.

KWA KUWA MPANGISHAJI ni mmiliki halali wa yard iliyopo, maeneo ya getifonga, ndani ya Halmashauri ya Manispaa ya Moshi.

NA KWA KUWA MPANGISHAJI ana nia ya kumpangisha MPANGAJI kwenye yard hiyo na Mpangaji anakubali kupanga yard hiyo.

HIVYO BASI MKATABA HUU UNASHHUDIA HAYA YAFUATAYO:-

1. KWAMBA, Mpangishaji atapangisha na Mpangaji atapanga yard kwa pango la shilingi laki tatu tu (300,000/=) kwa mwezi.
2. KWAMBA, Malipo ya kodi yatafanyika kwa mkupuo mmoja wakati wa kusaini mkataba huu na Mkataba huu utanza rasmi siku ya 01 mwezi wa 01 na mwaka wa 2024 na kumalizika tarehe 01 mwezi wa 01 2028.
3. KWAMBA, mkataba huu utadumu kwa muda wa miaka mitano kuanzia tarehe ya kusainiwa kwake na utaweza kurejewa baada ya kuisha pande zote mbili zitakaporidhia na kuingia makubaliano mapya.
4. KWAMBA, Mpangaji haruhusiwi kufanya marekebisho yoyote bila kutoa taarifa kwa Mpangishaji.
5. KWAMBA, gharama za bili za umeme, maji, taka na huduma zingine zihusizo nyumba zitachangiwa na Mpangaji. Mpangaji atalipia gharama za umeme kadri itakavyosomoka katika risiti za Shirika la umeme na akikaidi kulipia umeme atakatiwa. Aidha uharibifu wowote utakaosababishwa na matumizi mabovu ya umeme ya Mpangaji itakuwa juu ya Mpangaji kurekebisha.
6. KWAMBA, Mpangaji atawajibika kuweka yard na mazingira yake katika hali ya usafi kipindi chote cha mkataba na kuhakikisha kuwa yard inakuwa katika hali nzuri muda wote atakao kuwa kwenye mkataba. Aidha Mpangaji atawajibika kutunza na kuweka mazingira ya yard katika hali nadhifu na sal

ama.



7. KWAMBA, Mpangaji hatoruhusiwa kupangisha yard kwa mtu au kampuni yoyote ile bila kupata kibali cha maandishi kutoka kwa Mpangishaji.
8. KWAMBA, Mpangishaji atakuwa na haki ya kuingia na kukagua yard yake pale atakapoona inafaa kufanya hivyo.
9. KWAMBA, Baada ya mwaka mmoja kuisha Mpangaji na Mpangishaji atakuwa na uwezo wa kukaa chini kwa pamoja na kupitia upya vifungu vya mkataba huu kwa kufanya maboresho kadiri atakavyoona inafaa.

MAKUBALIANO haya yametiwa sahihi leo tarehe 01 mwezi 01 mwaka 2024 na wafutao:-


KWA KUSHUHUDIA MAKUBALIANO HAYA PANDE ZOTE MBILI ZIMEWEKA SAINI ZAO HAPA CHINI:

KWA USHUHUDA NA UTHIBITISHO MPANGAJI NA MPANGISHAJI.

Wamewekeana saini katika mkataba huu leo tarehe 01, mwezi wa 01 mwaka 2024 kwa namna kama inavyoonekana hapa chini.

KWA UPANDE WA MPANGISHAJI UMESAINIWA NA KUTOLEWA NA

JINA: JAMES MINJA

SAHIHI: 



KWA UPANDE WA MPANGAJI UMESAINIWA NA KUTOLEWA NA

JINA: THOMAS MSDFE

SAHIHI: 


MASHAHIDI WA MPANGISHAJI

JINA: NIXON RWEZAULA

SAHIHI: 



JINA: JESCA FELIX

SAHIHI: 




MASHAHIDI WA MPANGAJI

JINA: MUSA MSOFE

SAHIHI: M. Msufe

JINA: ZUTURA THANDU

SAHIHI: 

MAKUBALIANO HAYA YAMESAINIWA MBELE YA:

JINA: ESTERISA LAURAN

SAHIHI: 

CHEO: WAKILY

TAREHE:

